

KVTC

COMPANY HIGHLIGHT

# Uvyetishaji Misitu

na Joseph John

## Kwanini Uvyetishaji?

Uvyetishaji Misitu ni utaratibu wa ufatiliaji na uwekaji nembo wa mbao, miti na mazao yote yatokanayo na misitu, ambapo ubora wa usimamizi wa misitu unafanyiwa tathimini kulingana na viwango vilivyokubaliwa.

Uvyetishaji huu pia unaangalia hali za kijamii na kiuchumi za wafanyakazi na jamii husika huhusishwa katika maamzi ya uvyetishaji.

KVTC tunaamini kuwa programu ya uvyetishaji inasaidia utawala kuendelea kuboresha shughuli zetu na kuwa wasimamizi wazuri wa misitu, mazingira na usalama wa wafanyakazi wetu na watu ambao maisha yao yanaathiriwa na uwepo wetu

## Balaza la Usimamizi na Udhibiti Mazao ya Misitu

Baraza la usimamizi wa misitu ni shirika la kimataifa, lisilo la kibiashara, lenye wadau mbalimbali lilianzishwa mwaka 1993 ili kukuza uwajibikaji katika kusimamia misitu duniani. Shirika hili hufanya hivyo kwa kutengeneza viwango kwa mazao ya misitu ambapo uvyetishaji na uwekaji nembo vinakuwa pamoja.

KVTC imesajiriwa na mfumo wa udhibiti na mtiririko wa uzalishaji mbao. Usajiri huu unawahikishia wateja wetu kuwa mazao ya KVTC yanatoka sehemu halali na yenye misitu endelevu.

Wakati wa mkutano mkuu wa balaza la misitu huko Canada, wajumbe walipigia kura kuanzishwa mbinu mpya ya ubadilishaji wa misitu asili kuwa mashamba ya miti ambapo itafungua njia KVTC kusajiriwa na shirika la usimaizi wa misitu duniani.

## Viwango vya Kimataifa vya Mazingira, Afya Usalama Kazini


Mbali na uvyetishaji wa balaza la Misitu, Kampuni pia imesajiriwa kulingana na viwango vya Mazingira Afya na Usalama ambavyo vinatuongoza kupunguza athari za mazingira, kuwa na mazingira salama kwa wafanyakazi wetu na wakandarasi.

## Mawasiliano

Wasiliana na Meneja wa Mazingira, Afya na usalama kama una swali lolote kuhusiana na programu yetu ya uvyetishaji 0788 154 957, barua pepe jjohn@kvtc-tz.com

Tembelea pia www.fsc.org & www.iso.org

HIGHLIGHTS



## KVTC Teak in Tanzania

Tumeridhika kwamba mbao zetu za mitiki zinatumika kwenye mahoteli makubwa. Yakaribuni ilikuwa hoteli iliyo kamilika ya Jabal Ridge, Hifadhi ya taifa ya Ruaha ni moja ya hiyo miradi. Kwa kutumia mitiki, waendelezaji wana chagua malighafi endelevu katika ujenzi



## Yaliyo jiri kwenye Mfuko wa Jamii

Mwezi wa Novemba, Mfuko wa Jamii 2017 ulichangia millioni 71 kwenye vijiji shiriki. Nakwa mwaka 2017 miradi mipya kumi na moja ilianzishwa yenye thamani ya shilling milioni 154 za kitanzania karibu na 60% ya fedha ilitokana na mchango wa fedha za jamii.

# Kutoka Dawati la Hans

na Hans Lemm

Karibuni kwenye makala nyingine ya jarida letu. Nina matumaini utaiona ina taarifa unazoweza kuzitumia na kwa wale walioko kwenye "bonde la kilombero" tunatarajia mtasikiliza kipindi cha Redio Pambazuko Disemba 8!

Kama tunavyokaribia mwisho wa mwaka , tunaweza kuangalia nyuma juu ya mafaniko ya mwaka na licha ya hali ya changamoto ya kiuchumi Tanzania, tumeendelea kukua katika hisa la soko la ndani.

Kama sehemu ya jitihada inayoendelea ya kutokuwa na ajari tumepanga kutumia mifumo miwili ya kompyuta "PerForm" and "BeHave". Mifumo hii miwili itatupa muda halisi and taarifa za nyongeza juu ya mzizi wa sababu wa tukio na majeraha.

Uongozi wote wa kampuni ya KVTC unafanya jitihada ya maandalizi ya sherehe za miaka 25 na hatuwezi kusubiri kilele cha sherehe kitaka cho fanyika Disemba 20. Taarifa zaidi zipo kwenye makala ya jarida hili.

Tunasikitika sana kwa kifo kisichotarajiwa cha mpendwa wetu Dr William Shoo aliyefariki hospital ya St. Francis baada ya kuugua kwa muda mfupi. Tuna toa salamu za rambi rambi kwa familia yake.

Kama tulivyofikia mwisho wa mwaka wa mfungo na kujiandaa kwa msimu unaofuata wa mavuno. Tungependa kuwatakia furaha ya msimu na Baraka za 2018!





*Tukiongelea kuhusu KVTC , Mitiki na Sayansi ya Miti katika tukio la hivi karibuni Kampala, Uganda.*

**UNUNUZI KWA WAKUZAJI WA NJE?**

Tumeanza kununua mitiki kutoka kwa wakulima wa nje. Tafadhali wasiliana nasi 0713 376 817 au 0621 076 167

**TUSIKILIZE**

**Sikiliza Kipindi cha Mitiki Yetu**

Kwenye Radio Pambazuko 89.5FM

Kila Ijumaa 01.30 jioni na kila Jumamosi 01.30 asubuhi

**JE UNAJUA?**

Mtiki kwa mara ya kwanza uliingizwa Tanzania mwaka 1898 na watawala wa wakikoloni wa Wajerumani wakati huo ikijulikana kama Tanganyika

# Maazimisho ya miaka 25

na Kennedy Haule & Geofrey Kessy

KVTC ina sherekea kutimiza miaka 25 kwa kufanya shughuli mbalimbali zinazotuwezesha kuonyesha shughuli zetu za kibiashara, kubadilishana maarifa and kusherekea mafanikio ya miaka 25.

## ziara za viwandani

Kwenye tarehe 24, 25 na 26 mwezi oktoba. kvtc ilipokea viongozi wawakilishi wa vijiji shiriki kuja na kutembelea kiwanda na bustani ya kampuni kujifunza zaidi maandalizi ya upandaji lakini vilevile juu ya mnyororo wa uongozaji wa thamani, baada ya mavuno. Wengi wa jamii hawakuwahi kutembelea kiwanda toka kianze kazi 2010.

## Shindano la Insha

Mwezi wa September, tulianzisha shindano la insha kwa shule ya sekondari zilizoko kwenye vijiji shiriki vya kampuni. Jina la insha ilikuwa " "*Ni jinsi gani mazingira yangu yamebadilika tangu siku niliyo zaliwa na Mchango Wa KVTC ulivyochangia katika haya mabadiliko na mabadiliko gani ifanye kwa huko mbeleni*"

Shule nane zilileta insha 21 ili zipitiwe kwa zawadi ambayo itakabidhiwa katika tukio maalumu litakalo fanyika Kijiji cha mbasa Mwezi Novemba 30, 2017.

Mwandishi atapata zawadi ya shilling 115,000/= na shule nzuri itapata shilling 400,000. Matokeo yatapatikana kwenye mtandao.

## Uzito hai: uchafu au raslimali

Uchafu au raslimali ambayo ni matokeo ya shughuli za kiwandani ni "mabanzi" au "uzitohai". Hivi karibuni utaingia sokoni Tanzania kwa ubia na sisi kuangalia njia mbadala za kutumia uchafu huu

## Tarehe 20 Disemba

Tarehe 20 Disemba ni miaka 25 tangu kampuni ipande mti wake wa kwanza kwenye shamba namba D1 Mafinji na sasa imefikia umri wa kuvuna yote kwenye shamba hilo.

**WASILIANA NASI**

WASILIANA NASI AU TUANGALIE:
kvtc@kvtc-tz.com / http://kvtc-tz.com/

PO Box 655, Ifakara, TZ

PO Box 12452, Dar es Salaam, TZ